

**SHIRIKA LA ROZARI HAI MTANDAONI -TANZANIA**

**NOVENA YA KWANZA KWA MT. FILOMENA**

**TAREHE 02-10 JANUARI 2022**

**NIA:**

**1.Kumshukuru Mungu kwa zawadi ya Mwaka Mpya**

**2.Kuomba msaada wa maombezi ya Msimamizi wetu Mtakatifu Filomena Shahidi na Mtenda Miujiza atusimamie vema katika mambo yote.**

**3. Nia Binafsi**

**Mwanzo: Kila siku anza na sala ya Kutubu, Sala ya uje Roho Mtakatifu**

**Mwisho: Sali Sala ya Tunakimbilia Ulinzi Wako**

## JESHI LA MTAKATIFU FILOMENA

Njia nzuri na thabiti kabisa ingawa hutumiwa mara chache katika kuonyesha heshima kwa watakatifu ni kuiga fadhila zao na kwa kufanya hivyo tunapata mastahili ya maombezi na msaada wao pamoja na furaha ya milele. Tunapenda kushiriki furaha zao bila kushiriki mateso yao waliyopitia. Tukiwa na shauku ya kumfurahisha Mtakatifu Filomena katika njia yetu tutafakari maisha yake tukiwaza mateso yake na kufanya tafakuri ya kifo chake cha kishujaa. Sali ukimuomba akujalie mwanga na neema ya kutumia fadhila alizokuwa nazo katika hali yetu ya maisha. Tuwe na ujasiri wa kuondoa vilema vyetu na tabia mbaya ambazo ni kinyume na fadhila zake wakati tukijitahidi kuishi tabia zinazokamilisha fadhila zile ambazo kwazo mtakatifu Filomena anaheshimiwa.

**Siku ya Kwanza.**

Mtakatifu Filomena aliishi hapa duniani. Mimi pia ninaishi hapa duniani. Oh! Angalia tofauti kubwa iliyopo katika maisha yangu na maisha yake. Yeye alijiondoa kabisa katika malimwengu. Mimi nimejifunga mnyororo kujishikamanisha kabisa na malimwengu na sheria zake na uchafu wake na matumizi yasiyofaa ya mambo ya dunia hii. Je, ,mimi si nina shauku ya mambo ya kidunia na ninataka kujipatia sifa kwa mambo haya? Izo halNgoja nikate shauri la kuacha starehe zote ambazo zinahatarisha roho yangu na nifanye pia leo sadaka ya kukataa hata starehe zilizo halali.

**SALA:** ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina.***

**Siku ya Pili.**

Nina njia elfu elfu za kujitakatifuza ambazo Mtakatifu Filomena hakuwa nazo ili kurahisisha njia ya kuishi maisha ya fadhila. Naweza kujilinganisha mimi na Mtakatifu? Mungu anisamehe kwa namna nilivyotumia vibaya neema nilizojaliwa! Ni mara ngapi nimehoji mapenzi ya Mungu? Ni mara ngapi nimehoji ukarimu wake na hata mapendo yake kwangu? Angalia Imani yangu kwa Mungu ilivyo dhaifu na matumaini yangu kwake yanavyoondolewa. Ni mara ngapi nimeshindwa kutoa Shukrani kwa baraka zake na upendeleo anaonipa? Mtakatifu Filomena nipatie kutoka kwa Mungu neema ya kipekee ya kumwamini Mungu. Leo nifanye maamuzi ya kumshukuru Mungu kila siku kw amambo mengi lakini madogo madogo anayonijalia katika maisha.

SALA: ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina.***

**Siku ya Tatu**

Mtakatifu Filomena aliweka nadhiri ya ubikira. Alikataa raha na starehe za mwili na matumaini ya sifa zisizo za kweli. Nadhiri hii ilimwondolea raha za maisha lakini ikampa

taji la kifalme. Mtakatifu Filomena alitafakari; *“Itafaa nini ?dunia yote si kitu ukilinganisha na kiwango kidogog kabisa cha ukamilifu ambacho roho yangu itapata kwa sadaka hii? Ni vizuri sana kubakia daima mali ya Mungu,”* Angalia ukarimu huu! Angalia sadaka hii! Ni kauli ya heshima kabisa. Je ninafahamu thamani ya usafi? Mimi bado ni bikira? Kuna maadui wengi mno wa fadhila hii wanoonekana na wasioonekana wanaotaka kuniondolea fadhila hii. Nimeitunza fadhila hii kwa unyenyekevu, adabu, sala na kupokea sakramenti mara kwa mara? Kama nimeingia kwenye muungano mtakatifu wa ndoa, nimeheshimu ukuu wa sakramenti hii? Leo nitafanya jitihada maradufu kutunza fadhila hii kwa kuvaa mavazi ya staha na kuchunga macho yangu. Nitasali Salamu Maria tatu na kumuomba Bibi yetu anisaidie kulinda usafi wa mwili, roho na moyo. Nitaangalia mavazi yangu niondoe yale yote ambayo yanakosa adabu na kwenda kinyume na fadhila hii ambayo Mtakatifu Filomena aliitetea hadi kifo.

SALA

***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina.***

**<u>Siku ya Nne.</u>**

Mtakatifu Filomena alikataa mambo yanayovutia sana ya ulimwengu huu. Aliyaelewa vema maneno ya Solomoni. “*Ubatili mtupu!”*. Hakuridhika tu kuyaelewa bali aliyaishi katika wakati mgumu sana lakini wenye utukufu kwenye maisha yake. Aliyapuuza mambo ya kidunia. Kwa kutolea sadaka yote! Mtakatifu Filomena alipata kila kitu. Angalia mimi nilivyo katika hali mbaya! Ninatafuta mambo yote. Nimejinyima mwenyewe mambo mazuri ambayo hayo tu ndio yanatakiwa kupendwa na kuheshimiwa. Nimesadiki kwamba dunia pamoja na umaskini wake wote, ina uwezo wa kuwatajirisha wale wanaoitumikia na upuuzi wake eti unaweza kuniongoza katika utukufu! Nimeamini eti kuridhisha tamaa zangu kunaweza kunipa mimi furaha ya kweli. Mjinga mimi.

Makosa yangu yananiweka katika hatari, kwani si imeandikwa kwamba marafiki wa dunia hii ni maadui wa Mungu? Ni wakati wa kubadili mtazamo wangu wa giza na kuiona dunia jinsi ilivyo na kuitumia kama vile siitumii. Kudharau yale ambayo nilidhani ni ya maana na kutojishikisha na chochote isipokuwa upendoi. Nisamehe Eee Mungu wangu kwa ujinga wangu wa nyuma. Mtakatifu Filomena nisaidie kurekebisha maamuzi yangu, kuachana kabisa na malimwengu, na hata nikubali kwa furahaa kutoa sadaka ya chochote endapo

Mungu atanitaka nitoe sadaka hiyo kutoka kwangu. Leo jifunze uvumilivu/saburi katika yote yanayonihangaisha na kunisumbua na kuharibu ratiba zangu. Jipe muda wa kusaidia mhitaji.

SALA: ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina.***

**<u>Siku ya tano</u>**

Mtakatifu Filomena aliteseka mateso makali sana kwa ajili ya Mungu. Alikuwa binti mdogo, kutoka ukoo wa kifalmena hakuwa katika mateso yoyote kwa wakati huo. Ili aendelee na maisha haya ya furaha na mazuri alitakuwa tu kuficha dini yake na kuvunja nadhiri aliyofanya katika ujana wake ili kulinda maisha yake dhidi ya hasira ya Dioclesian. Maisha yake naya wazazi wake yangeweza kuokolewa kama angemkana Mungu. Mimi nafikiria nini kuhusu ujasiri kama huu? Nimeshawahi kuwa na mbegu kama hii ya ujasiri katika moyo wangu? Labda niko mwaminifu kwa Mungu sasa kwa sababu hainigharimu sana. Je siku gharama ya utii wangu kwa Mungu ikiwa kubwa nitaweza kubakia imara bila kusaliti Imani yangu? Na je ninaweza kusema kwa hakika kwamba kwa kufanya hivi nitafikia mwisho wenye furaha? Jambo hili haliwezekani endapo kama mkristu siwi au kuonekana mkristu kweli. Haliwezekani endapo sitamfuata Yesu Kristu kwa uaminifu na kubeba msalaba wangu kama Yeye alivyobeba msalaba wake. Basi ngoja nikubali kuteseka kwa hiari yangu mwenyewe. Wacha nitimize wajibu wangu wa kila siku vizuri hataka kama sikubaliani na mambo hayo. Ngoja nifutilie mbali mitazamo ya kibinadamu. Ngoja nijionyeshe mwenyewe, kila wakati na kila mahali kwamba mimi ni mkarimu na mtoto mwaminifu wa Maria. Leo nitaonyesha kwa uwazi na kukiri Imani yangug kwa kufanya moja au yote yafuatayo; *Nitafanya kwa uwazi ishara ya Msalaba, Nitaongea kuhusu Mungug kwa mtu nisiyemfahamu au kwa Rafiki, nitatembelea wagonjwa na kusali nao, nitavaa kwa uwazi rozari takatifu au mkufu wenye msalaba Unijalie Ee Mungu ninakuomba kwa mastahili ya Mtakatifu Filomena neema ya timiza maamuzi haya.*

*SALA:* ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea***

***msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina***.

**Siku ya Sita**

Mtakatifu Filomena alibakia jasiri bila ya kutikiswa mbele ya mateso ya kutisha. Wengi wanaanza lakini hawadumu. Mtakatifu Filomena alidumu katika njia aliyoianza hadi mwisho. Hakujali kuhusu yeye mwenyewe, hakusita, hakujuta, hakulalamika au kulaumu. Alikuwa amekubali "IWE KAMA UNAVYOTAKA" kama ile ya Bikira Maria pale alipopashwa habari na ile ya Mkombozi wake katika bustani ya Mizeituni. Hii ndio ilimlinda daima katika uamuzi wake na wito wake. Je, mimi niko imara bila kubadilika badilika katika mipango yangu ya kujitakatifuza? Au mimi ni wale ambao kwa saa moja ninaishi upande wa Mungu na siku nzima kwa ajili yangu mwenyewe na dunia? Endapo sitadumu katika njia sahihi, jitihada zangu hazitafuatiwa na ushindi. Mara elfu elfu nimeanza kwa roho lakini mara nyingi zaidi nimeishia kwenye mwili. Muda ule ninapoaga mambo ya dunia, muda huo huo ninanyoosha mkono kuyashika ya dunia tena! Na karibu kila ninapoacha ubatili wa dunia ninajifunga tena kwenye minyororo yake. *Ukigeugeu wa Kutisha. Tamaa isiyo na faida. Ee Mungu uniondoe katika hali hii ya ukigeugeu wa moyo! Mtakatifu Filomena nipatie kutoka kwa Mungu neema ya udumifu katika mema. Leo ninafanya maamuzi ya kutotoa neno la malalamiko kuhusu jambo lolote au mtu yeyote. Nitatafuta pia jambo jema la kusema kuhusu mtu niliyemuumiza hapo nyuma.*

*SALA:* ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina***.

**Siku ya Saba**

Mtakatifu Filomena alisaidiwa kwa uwezo mkubwa wa Mungu katika mapambano yake. Mungu atatusaidia katika magumu na vishawishi vyetu endapo tutamuomba. Atamtuma Yesu mwenyewe katika mikono ya Bikira Maria, mama yake, Malaika watakatifu, na Roho ya nguvu ndani ya mioyo yetu ili tuweze kuwashinda maadui wake na maadui wetu pia. *Hata nikiona jeshi lote limeungana dhidi yangu bado nitakuwa na matumaini.* Mtakatifu Filomena alipita bila woga na kwa ujasiri katika mateso na kifo. Je, mimi sio mtoto wa

Mungu? Je, Mungu hatafanya kwangu yale aliyofanya kwa Mtakatifu Filomena? Alas! Kwa nini ninakuwa na mashaka , kwa nini ninaogopa kwamba nitaachwa? Je, Mungu hakusema *"ombeni nanyi mtapewa?"* Je ninaamini kuwa kila asubuhi baada ya asubuhi Mungu ananipa Mwili wake mwenyewe na Damu yake katika Ekaristi Takatifu na bado ninashindwa kumuamini na kumtumainia wakati ninapoomba jambo dogo? Ondoa hofu hizi zisizo na sababu. Katika mahangaiko yangu nitamuomba Mungu kwa Imani thabiti, Mtakatifu Filomena Msimamizi wetu niimarishe katika nia zangu hizi . Leo muombe Mungu neema zote unazohitaji ili kupata wokovu wa milele.

*SALA:* ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina***.

**<u>Siku ya Nane.</u>**

Mtakatifu Filomena alivumilia mashambulizi yaliyofanywa dhidi yake. Ni kifo katika uwanja wa mapambano ndicho kilichompatia baraka za milele. Alishinda aibu na mateso ambavyo viwili hivi viliunganika bila mafanikio kumwondolea utukufu uliokuwa ume mmfunika kama vazi. Paza sauti yako! Ewe shahidi mashuhuri ! Njoo sasa uwaaibishe maadui wako wenye kiburi! Mapigo yao yamekuwaje? Mtakatifu Filomena alikufa na sasa anaishi. Alishindwa lakini sasa ni mshindi! Alidhalilishwa sana lakini sasa amekwezwa hadi juu kwa utukufu. Kudhalilishwa ni utangulizi wa utukufu, msalaba ni mdhamini wa furaha ya milele. Nimewahi kuyaelewa haya? Ninataka kuyaishi haya? Ingetokea nakutana na adui wa kutisha sana na kujitolea damu yangu kupambana naye, ningedumu kwa muda gani? Ingekuwa ni vita ya aina gani? Kuna wakati wa majaribu madogo ambayo kwa kweli ni kama sio kitu kabisa, halafu kuna uzito wa utukufu na heri na furaha zisizo na mwisho. Ee Moyo wangu jitanue katika Tumaini hili. Jambo hili halitanifanya nipokee tu vishawishi bali tu nitapokea vishawishi kwa furaha. Wacha macho yangu yatiririshe machozi maana kuna ahadi ya kupewa faraja ya thamani kubwa. Ee uchunggu usinikimbie maana baada ya uchungu furaha tamu inafuata. Naam, natamani kuteseka kusudi nipate furaha baadae. Natamani kupambana kusudi nipate ushindi. Natamani kunyenyekea na kunyenyekeshwa kusudi Mungu aniinue juu. Natamani kuifia dunia, kufia dhambi, kujifia mwenyewe kusudi niishi na Mungu na pamoja na Mungu kwa milele yote. Mtakatifu Filomena naomba univute

karibu yako na unisaidie kwa maombezi yako. Nihuishe na uniongoze kwa mifano yako. Nipatie neema ya kuifuata.

Leo fanya sadaka ya kutokula mlo mmoja au walau glasi ya maji wakati una kiu au njaa. Tiisha mwili wako kwa njia ndogo ndogo kwa ajili ya malipizi ya kujali mambo yako kuchukua nafasi ya Mungu kwa siku za nyuma na kwa ajili ya maandalizi ya kifo chako.

*SALA:* ***Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina***.

**Siku ya Tisa.**

Mtakatifu Filomena ni mwanga mpya kwa kanisa la Wapambanaji. Leo anashuhudia utume mtukufu. Kazi za watu wema hazipotei, ni mbegu zilizozikwa kwa kitambo kifupi tu. Kipindi cha baridi kali kimepita, Tunatangaza fadhila yake nzuri na ya kupendeza.. Njoo! Njoo! Ee Roho nzuri nay a kupendeza. Njoo ukae kati yetu. Mungu anaonyesha wema wake kwa wingi wa neema zake kupitia maombezi yako. Ilikuwa kama umande wa vinavyoonekana na visivyoonekana vikimpa Mungu sifa. Je, mastahili yako hayaendelei kuwa hai hata baada ya miaka mingi kupita? Mtakatifu Filomena amefanya nini ili kupata utukufu huu? Alipenda haki na kuchukia maovu. Moyo wake ulijaa mapendo kwa sheria ya Mungu. Ulilishwa na sheria hii usiku na mchana.. Kila alichokifanya kilituzwa mafanikio. Ngoja na mimi walau nianze kumfuata. Nitaanza kupanda katika shamba langu matendo ya fadhila. Kadiri mbegu zitakavyokuwa nyingi ndivyo pia mavuno yatakuwa mengi. Nitajitahidi kupata hazina ya fadhila, uvumilivu, mapendo na utii na fadhila zote za kikristo. Nitamtafuta Mungu pekee katika matendo yangu. Sitaruhusu fursa yoyote ya neema ipuuzwe Kwa msaada wako ewe binti wa kifalme uliyeko paradiso, Bikira na shahidi nitakusanya hazina kwa ajili ya kanisa linaloteseka, kanisa linalopambana na kanisa la washindi. Ninachokifanya kwa ajili ya Mungu ninakifanya kwa ajili yangu, kwa ajili ya Malaika, kwa ajili ya watakatifu, kwa ajili ya wenye haki na wadhambi. Ngoja nifanye haraka, wacha nisipoteze muda, . Nisaidie. Mtakatifu Filomena uwe egemeo la matumaini yangu, wewe uliyepewa jina lenye heshima kubwa la Msimamizi wa watoto wa Maria na Papa Pius IX unipatie ibada ya kweli na adilifu kwa Moyo Imakulata wa Maria, Malkia wa Rosari Takatifu.

***SALA: Salamu Ee Mtakatifu Filomena ambaye Mungu alikutukuza kwa miujiza mingi, Wewe ambaye Wakili wa Yesu Kristu alikutaja kuwa mlinzi wa Rozari Hai na wa watoto wote wa Maria. Onyesha sasa zaidi na zaidi kutoka huko mbinguni juu kwamba sauti takatifu kama yako haiwezi kukataliwa na tuna haki ya kukutegemea msaada wako. Tupatie neema ya kubakia waaminifu kwa Yesu Kristu hata ikitupasa kufa. Amina.***

Ewe Bikira mwaminifu na shahhidi mtukufu ambaye Imani yako ilishinda mashambulio ya dunia na motoni, Namtukuza Mungu kw aushindi wako na ninampa utukufu kwa nguvu ya ushindi aliyokupatia. Utukuzwe ee Mungug. Ee Mungu Mtakatifu. Ee Mungu unayestaajabiwa katika watakatifu wako. Ee Mungu mwenye haki, Mungu mwenye nguvu. Ee Mungu mwenye huruma isiyo na mwisho. Amina

*********AVE MARIA*************

*Imetafsiriwa na Juvenalis Ngowi Kwa kushirikiana na Fortunata Masaka. Inapatikana katika Kipeperushi cha Novena hii kilichotufikia kutoka Makao Makuu ya Rozari Texas USA mwaka 2020.*